# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

---

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

Ofisi ya Bunge

S.L.P 941

Dodoma

**APRILI, 2020**

# YALIYOMO

1.0 **UTANGULIZI** ........................................ - 2 -

2.0 **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 209/2020** ........................................ - 4 -

3.0 **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020** ........................................ - 5 -

3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ........................................ - 9 -

3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ........................................ - 10 -

4.0 **UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021** ........................................ - 11 -

4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ............ - 11 -

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ........................................ - 14 -

4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ................. - 16 -

5.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ........................................ - 18 -

5.1 FUNGU 37- Ofisi ya Waziri Mkuu ........................................ - 18 -

5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ................................ - 19 -

5.3 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ........................................ - 20 -

5.4 FUNGU 65 - Kazi na Ajira ........................................ - 20 -

5.5 FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi ........................................ - 21 -

6.0 **HITIMISHO** ........................................ - 22 -

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa kukuza ujuzi nchini **(Mradi Namba 6581, Fungu 65)** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020., uliotengewa **Shilingi Bilioni 18** na kupokea **kiasi cha Shilingi Bilioni 12** hadi Februari, 2020, ambacho ni sawa na **asilimia 66.7%** ya Fedha yote iliyoidhinishwa. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi hiyo, kwa Mafungu yote Sita (6) yaliyo chini ya Ofisi hiyo, tarehe 25 Machi, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Mafungu Sita (6) ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji ni kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na

vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha unaoisha;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 209/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambao kwa Mwaka wa Fedha 209/2020 ulitengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=).**

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa Fedha za kutekeleza Mradi huo, kwani kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Mbili (12,000,000,000/) sawa na asilimia 66.7% ya Bajeti ya Mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.***

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 25 Machi, 2020. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2019 na kiwango ambacho kimepokelewa kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020.

Aidha, uchambuzi huu ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi

Februari, 2020. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2019. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

## 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Tisa Kumi na Tatu, Laki Moja Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (40,913,154,200/=).** Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni**

**Mia Tatu Arobaini na Tatu, Laki Tisa Tisini na Tatu Elfu, Mia Tatu Themanini na Nane ( 27,343,993,388/=)** sawa na asilimia **66.8.**

Kamati, inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa mfano **bora na wa kuigwa na Wizara pamoja na Taasisi zote za Serikali katika kuongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ya Serikali, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.**

## 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake, katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Tatu na Milioni Ishirini na Moja, Laki Nne Elfu (73,021,442,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Nane Themanini na Moja, Laki Nne Tisini na Tano Elfu, Mia Tisa Tisini na Tisa (18,881,495,999/=)** zilikuwa za Mishahara, na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita, Milioni Mia Tatu, Laki Sita Arobaini na Sita Elfu na Hamsini na Tatu (26,300,646,053/=)** zilikuwa za Matumizi Mengineyo na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Nane Thelathini na Tisa, Laki Mbili Tisini na Tisa Elfu, Mia Tisa Arobaini na Nane (27,839,299,948/=)** zilikuwa za Ruzuku kwa Taasisi na Vyama vya Siasa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Mafungu hayo yalipokea jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Sita, Milioni Mia Nane Hamsini na**

**Nane, Laki Moja na Nane Elfu, Mia Sita Thelathini na Nane na Senti Sita (46,858,108,638.6/=) sawa na asilimia 64.2** ya bajeti. Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 2020 umeainishwa katika **Jedwali Na. 1** .

**JEDWALI NA. 1: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2020**

| NA. | FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 7,980,744,000 | 5,039,930,764 | **63.2** |
| 2 | 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 3,741,512,000 | 2,213,594,814 | **59.2** |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 23,671,461,000 | 16,852,477,550.35 | **71.2** |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,109,653,000 | 11,148,807,597 | **58.3** |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 5,234,294,000 | 4,392,584,795.25 | **84** |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 13,283,778,000 | 7,210,713,118 | **54.3** |
| | **JUMLA** | **73,021,442,000** | **46,858,108,638.6** | **64.2** |

***Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 25 Machi, 2020***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati ni kwamba hali ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

### 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020,

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu, ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni Hamsini na Sita, Milioni Mia Sita Thelathini na Saba, Laki Tano Sitini na Tano Elfu, Mia Saba Thelathini na Saba (56,637,565,737/=)** kwa ajili ya Miradi Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa Elfu (19,000,000,000/=)** zilikuwa ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa na Thelathini na Tatu Elfu, Mia Nane Thelathini na Nne (37,639,033,834/=) zilikuwa** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi Februari, 2020, jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Sabini na Sita, Milioni Mia Nne Arobaini na Tisa, Laki Nane Kumi na Nane Elfu na Thelathini na Saba (176, 449,818,037/=)** zilikuwa zimepokelewa, ambazo ni **sawa na asilimia 311.5** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji fedha ulifikia **asilimia 311.5** kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kupokea fedha za Kuboresha Daftari la Wapiga kura kutoka Hazina (**Fungu 21** - Wizara ya Fedha na Mipango), kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi, kiasi cha **Shilingi Bilioni Mia Moja Thelathini na Tisa, Milioni Mia Nne Hamsini, Laki Tatu Themanini na Tisa Elfu, Mia Tano Thelathini na Nane** (**139,450,389,538/=).**

**Mheshimiwa Spika,** ***Kamati imeipongeza Hazina kwa kutoa fedha za kuboresha Daftari la Wapiga kura kwa wakati, na imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Waziri Mkuu inavyoratibu Uboreshaji wa Daftari hilo kupitia Tume ya Uchaguzi, hatua ambayo imewezesha vijana wengi kujiandikisha na kupunguza kasoro nyingi zilizokuwepo hapo awali. Hivyo, hiyo ni dalili njema kuelekea Uchaguzi uliyo huru na haki kwa mwaka huu 2020.***

### 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 siyo wa kuridhisha kwa kuwa, Mfuko huo haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, **Maoni ya Kamati ni kuwa, pamoja na Vijana kuendelea kunufaika na Mikopo mbalimbali kupitia Halmashauri nchini, pamoja na Mradi wa kuongeza ujuzi**

**nchini, bado kuna kila sababu kwa Serikali kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Bajeti 2019/2020.**

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 tarehe 25 Machi 2020. Kamati imebaini kuwa, Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umeainisha maeneo 19 ya vipaumbele yakiwemo;

i) Kuchapa Nyaraka mbalimbali za Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa,

ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;

iii) Kuratibu na kusimamia Maendeleo ya Uwekezaji Nchini,
iv) Kuratibu na kusimamia Shughuli za Baraza la Taifa la Biashara,
v) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;
vi) Kusuluhisha Migogoro sehemu za Kazi,
vii) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji wa Maendeleo ya Vijana,
viii) Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini,
ix) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za Ajira za Watanzania nchi za nje,
x) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, na
xi) Kusimamia Taasisiza Umma zilizo chini ya Ofisi ya Wazi ri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba utekelezaji wa vipaumbele vyake ulenge zaidi katika kuboresha na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itatengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla hivyo, na kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya Nchi.**

4.2 **Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37),** Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa **(Fungu 27),** Tume ya Taifa ya Uchaguzi **(Fungu 61)** Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu **(Fungu 65)** zinatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Moja, Milioni Mia Moja Kumi na Nane, Laki Nane Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (41,118,854,200/=).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, Makadirio ya Makusanyo yanaongezeka kwa **Shilingi Milioni Mia Mbili na Tano, Laki Saba Elfu (205, 700,000/=)** ongezeko ambalo ni **sawa na**

**asilimia 0.5%** ya Bajeti ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuongeza Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa kuwa Ofisi hiyo imedhihirisha uwezo na ubunifu mkubwa katika ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali.**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali **Na.2.**

**Jedwali Na.2. Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Waziri Mkuu**

| FUNGU | TAASISI HUSIKA | MADUHULI YALIYOIDHINISHWA 2019/2020 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2020/2021 |
|---|---|---|---|
| 27 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 10,300,000 | 36,000,000 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 |
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 20,000,000 | 200,000,000 |
| 65 | Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu | 38,882,854,200 | 38,882,854,200 |
| **JUMLA** | | **40,913,154,200** | **41,118,854,200** |

***Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 25 Machi, 2020***

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Sita, Milioni Mia Sita na Saba, Laki Moja na Tatu Elfu (76,607,103,000/=)**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Tisa na Saba, Laki Tatu Thelathini na Tisa Elfu (17,907,339,000**/=) ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Thelathini, Milioni Mia Nane Thelathini na Tisa, Laki Moja Kumi na Saba Elfu, Mia Tisa Arobaini na Saba (30,839,117,947/=)** ni kwa ajili ya ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Vyama vya Siasa, na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Nane Sitini, Laki Sita Arobaini na Sita Elfu na Hamsini na Tatu (27,860, 646, 053/=)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Themanini na Tano, Laki Sita Sitini na Moja Elfu (3,585,661,000/=) sawa na asilimia 4.9%** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na ongezeko hilo la kibajeti ili kuiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza Majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo kuimarisha uratibu wa Masuala ya Uwekezaji nchini pamoja na Masuala**

**ya Vijana na Watu wenye ulemavu. Hii inatokana na Ofisi hiyo kuiridhisha Kamati kuhusu ilivyotekeleza Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa ufanisi mkubwa ndani ya Robo tatu ya Mwaka.**

### 4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Mia Mbili Kumi na Tisa, Milioni Mia Nne Sabini na Mbili, Laki Sita Ishirini na Tano Elfu (219,472,625,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Mia Moja Tisini na Nne, Milioni Mia Tatu Sitini na Nane Elfu (194,368,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Moja na Nne, Laki Sita Ishirini na Tano Elfu (25,104,625,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imeongezeka kwa **Shilingi Bilioni Mia Moja Sitini na Mbili, Milioni Mia Saba Thelathini na Tano, na Hamsini na Tisa Elfu, Laki Mbili Sitini na Tatu (162, 735, 059, 263/=).**Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 287.3%** ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko hayo katika Bajeti ya maendeleo pamoja na sababu nyingine muhimu, yanatokana na kuongezeka kwa Bajeti ya **Fungu 61 (Tume ya Taifa ya Uchaguzi)** kwa ajili ya kuiwezesha Menejimenti ya Uchaguzi ili iweze kutekeleza Majukumu yake yanayoikabili Mwaka huu wa 2020 kwa ufanisi mkubwa zaidi unaotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo Matano (5)** yakiwemo:-

(i) Kuendeleza ujenzi wa Makazi ya Mhe. Waziri Mkuu Mlimwa Dodoma;

(ii) Kuendeleza Mbegu za Mazao ya Kilimo na Uvuvi *(Agricultural and Fisheries Development Program);*

*(iii)* Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za Lishe *(Support Implementation of Nutritional Activities);*

(iv) Ujenzi wa Jengo Ia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma;

(v) Kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020;

(vi) Kuratibu na kukuza Kazi na Ajira za Staha Nchini;

(vii) Kutekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za kazi ya nguvu kazi nchini kwa ajili ya uchumi wa viwanda katika sekta za kilimo-biashara, utalii, usafirishaji,TEHAMA, madini, mafuta na gesi; na

(viii) Kuwajengea uwezo wa Kiuchumi Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## 5.1 FUNGU 37- Ofisi ya Waziri Mkuu

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Kamati imeridhishwa na uwezo wa Ofisi hii katika kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa lengo la kupunguza utegemezi. Hivyo, Serikali iendelee na jitihada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ikiwa ni pamoja na kumpata Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ambaye ni Mwanamke, ambaye amefanya mageuzi makubwa kwa kuboresha miundombinu na kuongeza Makusanyo

ya Serikali kwa kiasi kikubwa na kwa muda mfupi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua ya utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu kupunguza bajeti ya fedha za nje kwenye Miradi ya Maendeleo. Hivyo, Kamati inaendeleo kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa, fedha za ndani zilizotengwa zinapatikana kwa wakati kama zilivyoombwa. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaendelea kuongeza vyanzo vipya vya Mapato, kuboresha mazingira ya Uwekezaji nchini kwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza kasi ya Ujenzi na Uendelezaji wa Viwanda nchini, hatua ambayo itaongeza fursa za kiuchumi na kuongeza pato la ndani.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, iendelee kuimarisha Usimamizi wa Masuala ya Uwekezaji nchini kwa lengo la kuongeza na kuchochea ukuaji wa Uchumi wa Viwanda nchini kuelekea Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

## 5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuelekea Uchaguzi Mkuu, kuhakikisha inasimamia mwenendo wa Vyama vya Siasa kwa kuendelea kuchunguza na kufuatilia mienendo ya Vyama vya Siasa, ili

vizingatie Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi kwa ustawi wa Taifa letu.

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mienendo ya Vyama vya Siasa ikiwemo kuchukua hatua stahiki kwa kila Chama kinachovunja Misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria zingine za nchi, kwa lengo la kulinda Umoja, Udugu, Amani, Ulinzi na Usalama wa nchi yetu, kabla na baada ya Chaguzi zijazo.

## 5.3 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

i) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa chini ya Mfuko huu, Kamati inaendelea kushauri Mfuko uendelee kutoa Elimu ya kutosha kwa Waajili na Wafanyakazi hususan Vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajili wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajiandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri Mfuko kuweka na kuimarisha Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

## 5.4 FUNGU 65 - Kazi na Ajira

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi

(OSHA), Kamati inaendelea kushauri kuwa, OSHA iendelee kubuni mikakati endelevu na kuitekeleza kuhusu kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda nchini katika kulinda usalama wa Wafanyakazi.

ii) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na hatua ya Serikali ya kuanzisha Kitengo cha kuratibu masuala ya Watu wenye Ulemavu nchini ikiwemo kuanzisha Rasmi Baraza la Taifa la kuratibu Masuala ya Kundi hilo kwa ujumla, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inasimamia kitengo hicho na Baraza husika ili vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake kwa weledi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuendeleza hatua zake za kutatua migogoro mbalimbali inayoendelea katika Vyama vya Watu wenye Ulemavu nchini.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tamisemi, wahakikishe wanaongeza udhibiti wa marejesho ya Mikopo ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili Mfuko huo uwafikie Vijana wengi zaidi. Hatua hiyo iende sambamba na utoaji wa Elimu kuhusu matumizi bora ya fedha za Mfuko kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

## 5.5 FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

i) **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Kamati kuridhiswa na Utekelezaji wa ushauri wake kuhusu kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kwa uangalifu mkubwa, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujitahidi kufanya kazi yake kwa Weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa

Uchaguzi, na hasa kipindi hiki kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kushauri kwamba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa Uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria.

iii) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na jinsi Hazina ilivyotoa kwa wakati Fedha za kuiwezsha Tume ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Wapiga kura, bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatoa Fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wakati ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu masuala mbalimbali ya Uchaguzi kwa ufanisi Mkubwa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb), Waziri wa Nchi (Uwekezaji), Mhe. Angellah Kairuki, (Mb), Manaibu Waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), na Mhe.Stella Alex Ikupa, (Mb), Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana,Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**
3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;

4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb-Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb – Mjumbe,
21. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe

22 Mhe. Dkt.Suzan Alphonce Kolimba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndg.Gerald S.Magili, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo husika vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

1 APRILI, 2020